HALMASHAURI YA JIJI LA TANGA

SHULE YA SEKONDARI HORTEN,
S. L P 1522,
TANGA.

04/12/2017.

KUMB; NA. HSS/JNI/KID 1/2018.

JINA LA MWANAFUNZI: _____

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI HORTEN WILAYA YA TANGA MKOA WA TANGA MWAKA 2018.

UTANGULIZI:

Ninafuraha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2018.

Shule ya sekondari Horten ipo katika Kata ya Duga Magomeni **MWISHO KARIBU NA SHULE** ya Msingi Jaje.

Usafiri wa daladala kutoka mjini unapatikana.

Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe 08/01/2018. Unatakiwa kuripoti shuleni tarehe 04/01/2018 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 16/01/2018.

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

WAVULANA

a) Suruali mbili (2) mshono wa heshima siyo " modals", upana wa chini isipunguwe inchi 18. Suruali za kubana haziruhusiwi.
b) Shati mbili (2) nyeupe za mikono mifupi.
c) Viatu vyeusi vya kufunga kamba mbele.
d) Soski nyeupe.
e) Mkanda mweusi wenye bakozi ndogo ya kawaida na usiozidi upana wa icnhi $1^1/_2$ na usiwe wa maremborembo.
f) Picha mbili (2) za pasport size bachgbround ya blue akiwa amevaa shati jeupe.

WASICHANA

a) Sketi mbili (2) za marinda ya upanga.
b) Shati mbili (2) nyeupe za mikono mifupi.

c) Wale watakaovaa hijjab, washone sketi ndefu inayoishia kwenye vifundo vya miguu yenye marinda ya upanga na short kanzu. Short kanzu inatakiwa iwe ndefu usawa wa magoti na isiwe ya kubana.
d) Wale wasiovaa hijabu washone sketi zenye marinda ya upanga (mzunguko).
e) Soski nyeupe mbili, ziwe ndefu kufikia magotini.
f) Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga kamba mbele. Visiwe vya kisigino kirefu.
g) Kwa wale watakaohitaji sweta, liwe la rangi ya shule (kijivu) lenye shingo ya V.
h) Picha mbili za passport size, background ya blue akiwa amevaa shati jeupe.

NB:

- **Kitambaa cha sketi na short kanzu kiwe kinafanana.**
- **Sare za shule zinashonwa na mzazi/mlezi mwenyewe.**
- **Tafadhali mshonee mwanao nguo za heshima .**
- **Zingatia maelekezo kuepuka usumbufu usio wa lazima.**
- **Hatutawavumilia wale watakaokaidi maagizo.**

IKUMBUKWE KUWA MALEZI BORA NA TABIA NZURI KWA WATOTO HUANZIA NYUMBANI KWA WAZAZI.

Ili tufanikiwe, mzazi/mlezi unatakiwa kushirikiana na walimu pamoja na jamii kwa ujumla katika malezi ya mwanao kwa kipindi chote atakachokuwa hapa shuleni.

Mzazi ujenge tabia ya kuja shuleni mara kwa mara kujua maendeleo na mwenendo wa mwanao usisubiri kuitwa. Timiza wajibu wako.

VIFAA VYA DARASANI

Mzazi anapaswa kumpatia mwanao:

i. Begi kwa ajii ya kubebea vitabu na daftari.
ii. Daftari za kutosha (Counter books) masomo tisa (9).
iii. Kalamu (pen), penseli, kifutio na rula.
iv. Mkebe wa hesabu (Mathematical set).
v. Photocopy ya cheti cha kuzaliwa.
vi. Pesa ya matumizi yake binafsi awapo shuleni.
vii. Nauli ya kwenda na kurudi shuleni kadri ya umbali anakoishi.

MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE.

a) Wizi.
b) Uasherati na ushoga.
c) Ubakaji .
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama uvutaji bangi,cocaine, mirungi, sigara nk.
e) Kupigana au kupiga.
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
g) Kudharau bendera ya Taifa.
h) Kuwa mja mzito/ kupata maimba.
i) Kuoa au kuolewa.
j) Kutoa mimba.
k) Kugoma,kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule na watu.
l) Kukataa adhabu kwa makusudi.
m) Kuwa na simu ya mkononi.

NB: Mwanafunzi yeyote atakayekamatwa na simu shuleni, atatakiwa kuivunja yeye mwenyewe mbele ya mzazi wake na wanafunzi wote.

MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI.

a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali. Form hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara atakaporipoti shuleni.
b) Form ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
c) Form ya mzazi ya kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

TAFADHALI SOMA KWA MAKINI MAELEZO/MAAGIZO HAYA NA KUYATEKELEZA KIKAILIFU.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

……

EUGENIA KINAMBOI

MKUU WA SHULE

KWA MZAZI/MLEZI:

KUTAKUWA NA KIKAO CHA WAZAZI TAREHE 04/01/2018 SAA 2:00 ASUBUHI HAPA SHULENI. FIKA BILA KUKOSA UKIWA NA MTOTO WAKO NA UZINGATIE MUDA.

MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

SEHEMU HII IJAZWE NA MWANAFUNZI

1. Jina kamili la Mwanafunzi kwa kadiri ya matokeo ya darasa la saba _____
2. Tarehe ya kuzaliwa : _____
3. Sehemu ulipozaliwa : _____
4. Dini/Dhehebu : _____
5. Utaifa _____
6. Darasa ulilomaliza : _____
7. Anuani ya shule uliyotoka: _____
8. Jina la mzazi: i)Baba _____simu _____ Hai / Amekufa _____
   ii)Mama_____ simu_____ Hai/ Amekufa_____
9. Kazi ya Mzazi: i) Baba_____
   ii) Mama_____
10. Wategemezi wengine wawili, anuwani kama hana wazazi na namaba ya simu.

Anuani ya tegemezi : _____
Jina la atayegharamia mahitaji yako ya shule:_____
Anuani yake: _____
Namba ya simu :_____
Uhusiano _____ (Kaka,dada,mjomba nk)

Sehemu anayoishi Jijini Tanga:
Mtaa _____
Jina la Mwenyekiti wa mtaaa:_____
Sdahihi yake na muhuri :_____

SEHEMU HII IJAZWE NA MZAZI / MLEZI

Mimi _____ Mzazi / Mlezi wa _____
Nakubali ajiunge na Shule ya Sekondari Horten na ninaahidi kumpa mahitaji yote ya shule kama inavyotakikana. Ninaahidi nitamtunza na kushirikiana na shule kumlea kitabia na kimaadili.

Sahihi _____
Tarehe _____

UTHIBITISHO WA KATIBU MTENDAJI WA KATA.
Mim _____ambaye ni Afisa mtendaji **WA KATA YA** _____
Nathibitisha kwamba kwa kadiri ya uwezo wangu maelezo aliyotoa mwanafunzi katika maelezo binafsi ya mwanafunzi ni ya kweli.

Sahihi: _____ Simu _____ Tarehe :_____

Muhuri :

SHULE A SEKONDARI HORTEN

SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

HESHIMA

1. Mwanafunzi anatakiwa kuwa mfano kwa kuwa na heshima na adabu ya kiwango cha haki ya juu.
2. Mwanafunzi anatakiwa kusimama na kusalimia mwalimu au mtu yeyote mwenye umri mkubwa anapopita.
3. Mwanafunzi hatakiwi kutumia lugha mbaya wakati wowote.
4. Mwanafunzi anatakiwa kuwaheshimu wafanyakazi wote walioko shuleni.

NIMWIKO KWA MWANAFUNZI

1. Kuvuta sigara au tumbaku.
2. Kufuga nywele na kucha ndefu.
3. Kufuga ndevu.
4. Kuvaa mavazi yasiyo na heshima mfano / sketi za kubana / viatu vya wazi nk.
5. Kunywa pombe.
6. Kutumia madawa ya kulevya.
7. Kupigana.
8. Kuwa mchafu.
9. Kuacha kufanya mitihani / majaribio bila sababu ya msingi.
10. Kuja na simu shuleni.

KUWAHI:

1. Mwanafunzi anatakiwa kuwahi katika shughuli zote kama zilivyopangwa katika ratiba ya shule.
2. Mwanafunzi anatakiwa kuwahi anaposikia wito wa dharura.
3. Mwanafunzi anatakiwa kuwahi shule saa 12:30 asubuhi kwa siku zote za masomo.

MAHUDHURIO

1. Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria vipindi vya masomo ndani na nje ya darasa kwa muda wote wa masomo
2. Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria mikutano yote ya shule,kama paredi ya asubuhi, mikutano ya darasa nk.

SARE

Uvaaji wa sare ni lazima kwa mwanafunzi:

1. Wakati wa masomo darasani.
2. Unapokwenda Hospitali.
3. Unapotoka au kurudi nyumbani kutoka shule.
4. Kwenye sherehe za shule, za kitaifa na ziara za masomo.

GOVERNMENT OF TANZANIA

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

HORTEN SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 1522,
TANGA.

TO:
MEDICAL OFFICER.

RE: _____name in full).

Please examine the above named as to his / her physical and mental fitness for a full time school course. The examination should be include the following categories (I – III).Each category will reader the applicant in eligible in case of defect. Pregnancy (Category IV) will also render girl a girl candidate ineligible for the course.

I. (a) Eye sight (b) Limbs (c) Hearing (d) Speech
(e) Venereal Diseases (f) Leprosy (g) Epilepsy

II. Neuroses

III. Other serious diseases

IV. Pregnancy

Signature :

PART B:
MEDICAL CERTIFICATE
(To be completed by Government Medical Officer)
I have examined the above named and consider that he / she is physically fit / unfit and mentally fit/ unfit for a full time schooling course.

I. (a) Eye – sight _____
(b) Hearing _____
(c) Venereal diseases _____
(d) Epilepsy _____

II. Neuroses _____

III. Other serious disease _____

IV. Pregnancy _____

Station _____ Signature _____

Doctor's name _____ Designation _____

Date _____

Delete where necessary STAMP

HALMASHAURI YA JIJI LA TANGA

SHULE YA SEKONDARI HORTEN,

S.L.P. 1522,

TANGA.

FOMU YA KUKUBALI NAFASI ULIYOPEWA.

AHADI YA MWANAFUNZI.

Mimi _____ SIKUBALI / NAKUBALI nafasi niliyopewa katika shule ya sekondari Horten.

KWA YULE ANAYEKUBALI TU:

Naahidi kuwa kuwa nitatii kanuni na sheria zote za shule. Nitafuata masharrti yote yatakayotolewa na Mkuu wa shule , Walimu na Viongozi wa Shule.

Ninaahidi pia kuwa nitashirikiana na wanafunzi wenzangu katika shughuli za masomo, kazi za nje na katika michezo kwa muda wote nitakaokaa HORTEN SEKONDARI.

MWANAFUNZI MZAZI/MLEZI

Sahihi: _____ Sahihi: _____

Tarehe :_____ Tarehe :_____

MAPINDO YA UPANGA YANYOOKE